ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.

23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.

34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.

48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
59.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
62.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
63.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
64.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
65.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
66.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.

68.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
69.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
70.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
71.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
72.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
74.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
75.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
76.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Kumi – Tarehe 28 Oktoba, 2009

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Ali Mzee Ali) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Nam. 8 ya 1999. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Nam. 8 ya 1999. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mohammed Ali Salim (Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Upande wa Upinzani kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Nam. 8 ya 1999. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 63

Mradi wa Kuzoa Taka Wilaya ya Magharibi

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Halmashauri ya Magharibi ilianzisha mradi wa uzoaji taka katika maeneo ya Mombasa, Chukwani na kadhalika na kulipa shilingi 2,000 kwa nyumba na shilingi 6,000 kwa wenye maduka. Lakini kwa hivi sasa zoezi hilo limetanua wigo wake na sasa pia kwa wenye maduka ya kuanzia Kwa Nyanya, Kihinani, Bububu, Mtoni n.k. na wao wanalipa shilingi 6,000 kwa wote wanaofanya biashara ya duka hata la mitumba/nguo.

(a) Je, Mhe. Waziri suala hili unalifahamu?

(b) Kwa kuwa leseni za biashara ya maduka zinapitana. Je, ni maduka yepi yanayolipa shilingi 6,000?

(c) Je, ni kweli kuanzia Kwa Nyanya kuja Mtoni wamo katika mpango huo?

(d) Je, mradi huu unafanywa na Halmashauri yenyewe au Kampuni?

(e) Je, kuna taaluma yoyote iliyotolewa kwa wafanyabiashara na wananchi kabla ya kuanza zoezi hilo?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 63 lenye vifungu (a), (b), (c), (d) na (e) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti,

(a) Serikali inalifahamu zoezi la uzoaji taka linalofanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi.

(b) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa viwango vya leseni za biashara vinapishana. Kwa mfano, wenye maduka ya vifaa vilivyotumika *(used)*, maduka ya vioo, gereji, bekari, maduka ya vyakula ya jumla, wapiga matofali kwa mashine na wakosha magari wanalipa shilingi 6,000 kwa mwezi. Wenye maduka ya mitumba na maduka madogo madogo ya nguo shilingi 3,000 kwa mwezi. Aidha yapo maduka mengine ambayo hulipiwa shilingi 4,000 au shilingi 5,000 kulingana na ukubwa wa duka na mtaji.

(c) Kwa sasa zoezi la kuzoa taka linafanyika katika Shehia za Tomondo, Mombasa, Pangawe, Mwanakwerekwe na Melinne. Pia kwa kutumia gari maalum la kukodi, lipo zoezi la kupita na kuchukua taka katika maduka yaliyomo kando kando ya barabara kuanzia Chukwani hadi Bububu na Kihinani. Kwa upande wa Kwa Nyanya mpaka sasa kilichofanyika ni uhamasishaji kwa wafanyabiashara kujiunga na mpango huu. Nao kimsingi wameshakubaliana na mpango huu. Kuanzia tarehe 10/10/2009 gari la taka limepewa agizo la kufika eneo la Kwa Nyanya kubeba taka zao.

(d) Kwa sasa mradi huu unafanywa na kusimamiwa na Halmashauri yenyewe tangu tarehe 18/11/2008 baada ya Kampuni ya *Mic Tax Commission Agent* iliyokuwa wakati wa uzoaji taka kushindwa kufanya kazi hiyo.

(e) Kabla ya kuanza zoezi hili wananchi na wafanyabiashara walielimishwa na kuhamasishwa katika mikutano mbali mbali ndani ya Shehia zao. Pia ziara za kupitia nyumba kwa nyumba zilifanyika ili kuhakikisha kuwa kila mwananchi amepata taaluma hiyo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi kwa kuanzisha mpango huu wa kuondoa adha ya taka katika maeneo yetu. Kwa maeneo ambayo wafanyakazi wamejitokeza wengi na wanaendelea vizuri kuna eneo la Mwanakwerekwe, hawa wenzetu wanafanya kazi nzuri na uvivu wako ndio utakaokusababishia taka zibakie.

Kwa kuwa mpango huu wananchi wameuridhia kwa kila nyumba kulipa shilingi 3,000 katika maeneo haya yanayozolewa taka na hakuna manung'uniko kwa sababu kazi inafanyika. Kwa kuwa mtandao mzuri huu umeonesha dhahiri kwamba mji wetu unakuwa katika mazingira mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maeneo ambayo kayataja Mhe. Waziri, lakini kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi ni kubwa na adha ya taka ni moja katika chanzo cha kuleta maradhi mbali mbali. Je, Mhe. Waziri ana mpango gani wa makusudi kupitia Halmashauri kuelekeza nguvu kwa maeneo yale ambayo bado haujafika mpango huu?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Mwenyekiti, pongezi alizotoa Mhe. Mwakilishi tumezipokea na kama tujuavyo kabla ya kuanzisha shughuli hii ni kuanza kufanya survey kupitia nyumba kwa nyumba kuwaelimisha watu. Zoezi baada ya kufahamika ndio hapo shughuli ya kuzoa taka inapokuwa inaanza.

Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi, waheshimiwa wajumbe, pia wanahitajiwa kutoa msukumo au maelekezo pale watakapopata nafasi ya kuzungumza na wananchi. Kwa sababu usafi wa mji wetu ni usafi kwa nchi nzima.

Mhe. Mwenyekiti, swali la pili, Wilaya ya Magharibi kama tujuavyo ni kubwa mno kulingana na Mkoa wa Mjini Magharibi, lakini taka katika Mkoa wa Mjini Magharibi zitakuwa ziko nyingi zaidi kuliko Wilaya ya Magharibi. Hata hivyo,

tujaribu kuwahamasisha wananchi wetu wanaokaa sehemu ya Magharibi ili zoezi hili liweze kufanikiwa.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amekiri kwamba lipo zoezi la kuzoa taka maeneo ambayo niliyataja Kwa Nyanya, Kihinani, Bububu, Mtoni n.k na amesema kunategemea leseni za biashara na ulipaji huo.

(a) Kwa kuwa taka zikizolewa zinatupwa kwenye jaa maalum ambalo ni Jumbi na eneo hili hivi sasa limejaa na tulisikia wizara inatafuta eneo jengine. Je, zoezi hili limefikia hatua gani?

(b) Nasikia nchi zilizoendelea kwamba kuna magari maalum zikitiwa taka zinachomwa mle mle na baadae zinakuwa hazileti athari kubwa kama ilivyo taka za kutupa kwenye jaa kubwa. Je, suala hili serikali imelizingatia vipi?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Mwenyekiti, magari ya taka ya aina hiyo ni kweli yapo na wenzetu ndio wanayoyatumia kwamba taka zinapotiwa katika hayo magari huwa zinachomwa mle mle, sehemu ndogo inayobakia ndio inakwenda kutupwa.

Kwa ujumla zoezi tumejaribu kulifanya kwa utaratibu utakaoeleweka na tunakwenda hatua kwa hatua. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, zoezi linaendelea vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni la utupaji taka. Kama serikali ikipata uwezo mzuri na kuagiza magari haya, hili zoezi la utupaji taka litakuwa limefanikiwa.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, jaa la Jumbi ambalo lilikuwa likitupwa taka na Halmashauri ya Wilaya pamoja na Baraza la Manispaa Zanzibar limejaa. Kinachoendelea hivi sasa, taka hizo za Halmshauri ya Wilaya pamoja na Manispaa husambazwa katika Wilaya ya Kati hasa katika jimbo langu mimi la Koani katika maeneo ya uwanda wa Tunguu, Binguni na Jumbi.

(a) Je, Mhe. Waziri haoni hii ni hatari hasa katika siku hizi tunazoendelea nazo za mvua kwamba hivi sasa wananchi wameshakuwa wanapata bughudha ya nzi na harufu mbaya katika maeneo hayo?

(b) Katika utaratibu huo haoni iko haja hayo magari ya kuchoma taka yakaletwa haraka haraka ili kutunusuru watu wa Jimbo la Koani kutokana na maafa ya kutupiwa taka?

(c) Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi inakusanya taka, lakini baadhi ya taka hizo hutupwa Mbuyu Mnene eneo la Uwanja wa Ndege ambapo husababisha kunguru na wanyama wengine kusambaza uchafu huo. Je, Mhe. Waziri atachukua hatua gani kuona taka hizi zinazozolewa katika eneo hilo hazitupwi hapo na kuweka usalama katika Uwanja wa Ndege?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza swali la Mbuyu Mnene kwamba zinatupwa taka kwa Wilaya nzima ni taka ambazo zinapita, zinamwaga zinakuja kuondoshwa, lakini sio kama vile ilivyokuwa inafanywa Jumbi, yaani zinatupwa taka kwa kiwango kikubwa na kushindiliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la magari ili kunusuru usambaaji wa taka, hilo suala tunajaribu kulifanyia kazi na tukiweza kupata magari mawili matatu yataweza kutoa msaada katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kumwaga taka sehemu mbali mbali kama vile Tunguu, Jumbi na Binguni, hilo zoezi wengine huwa wanaomba wao wenyewe taka zile wakatupiwe kwa sababu ya masuala ya kilimo. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi ni muhimu awaelimishe wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, utupaji mwengine wa taka ni kwamba baada ya kushawishiwa wananchi wao wenyewe kuona kwamba michungwa, miembe na miti mingine inafaidika na umwagaji taka katika sehemu mbali mbali za kisiwa chetu.

Nam. 42

Elimu kuhusu Sera ya Elimu ya Vijana

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Katika jitihada za kuona kwamba wadau wa maendeleo ya vijana wanaitambua na kuielewa vyema “Sera ya Maendeleo ya Vijana” Idara kwa kushirikiana na Jumuiya ya *Zanzibar Youth Forum* imeendesha mafunzo mbali mbali kwa Jumuiya na wadau wa maendeleo ya vijana kwa kila Wilaya. Mafunzo hayo yalilenga zaidi kuchambua na kujadili vipengele na matamko mbali mbali

yaliomo katika Sera ya Maendeleo ya Vijana na kuyatolea ufafanuzi na kuyafanyia uchambuzi wa kina ili yaweze kueleweka kwa urahisi.

(a) Je, Mhe. Waziri mafunzo hayo yalitolewa katika ngazi ya Wilaya yalishirikisha vijana wangapi kwa kila Wilaya?

(b) Kwa kuwa sera hiyo ya maendeleo ya vijana bado haijaeleweka kwa kundi kubwa la vijana ambao ndio walengwa. Wizara ina mikakati gani katika suala hili?

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mafunzo ya Wadau wa Maendeleo ya Vijana juu ya Sera ya Maendeleo ya Vijana yaliandaliwa kwa mashirikiano kati ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya *Zanzibar Youth Forum.*

Mhe. Spika,

(a) Mafunzo hayo yalishirikisha vijana 30 kutoka kila Wilaya za Zanzibar.

(b) Ili kuifanya Sera hiyo kueleweka kwa vijana wengi, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *UNICEF* imechapisha nakla 2,000 zaidi baada ya kujitokeza upungufu wa vitabu vya Sera hiyo, ili vigawiwe kwa vijana. Aidha, inapofanyika Mikutano, Semina au Makongamano ya Vijana suala la kuelimisha Sera linapewa kipaumbele. Wizara pia kwa kushirikiana na *UNICEF* imeunda Kamati ya Kufuatilia Utekelezaji wa Sera hiyo ambapo kamati hiyo inashirikisha Wadau kutoka Taasisi za Vijana zikiwemo zile za Serikali na hata zisizo za Kiserikali, kwa lengo la kutoa elimu ya Sera hiyo na kuhamasisha utekelezaji wake.

Nam. 69

Upunguzaji wa Masharti ya Mikopo ya Pesa za Mhe. Rais

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto imekabidhiwa dhima ya kuvipatia mikopo itokanayo na fedha za Mhe. Jakaya Mrisho

Kikwete na Amani Abeid Karume vikundi mbali mbali vya wananchi ili waweze kujinasua na umasikini wa kipato unaowakabili. Hata hivyo, cha kushangaza ni pamoja na kuchelewa kwa fedha hizo.

(a) Je, Mhe. Waziri, Wizara yako ina mkakati gani wa kupunguza masharti ya mikopo hiyo ili kupunguza urasimu wa kupatikana kwa fedha hizo kwa wakati?

(b) Hivi Mhe. Waziri kuna mchango wowote wa fedha unaotolewa kwa vikundi hivi ili vipatiwe mkopo huo?

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inapokea maoni na kutathmini matatizo yanayojitokeza katika mchakato wa mkopo nafuu na kamati husika ya kisekta iliyoundwa inatafakari na kujitahidi kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayojitokeza.

(c) Hakuna mchango wowote wa fedha unaotolewa kwa vikundi kwani mkopo huu tayari una sura ya unafuu.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri ni mtoa ushauri wa mfuko huu wa masharti nafuu kama alivyoeleza. Kwa kuwa tokea ulipoletwa umekuwa na kipindi kirefu baadhi ya walengwa wameshapewa, wameshatia faida na wamesharejesha kama wenzetu wa Tanzania Bara.

Je, Mhe. Waziri atanambia nini kulingana na vikundi vya ushirika au *SACCOS* za hapa Zanzibar na hasa Wilaya ya Mjini ambayo ni majimbo 10 kuwa mpaka leo baadhi ya vikundi vingi vya ushirika havijapata mkopo huu wakapata kujinufaisha kimaisha?

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kumfahamisha kwamba mkopo huu nafuu wa Marais wetu haukuanza kutolewa kwa wakati mmoja, wenzetu wa bara walitangulia na sisi tukafuata baadae.

Mhe. Mwenyekiti, la pili katika swali nitakalolijibu baadae nitaonesha ni kiasi gani kimetumiwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Lakini pia kama tulivyoelezwa huko nyuma kuna matatizo yanayojitokeza katika ujazaji hizo fomu ndio unaofanya kwa sehemu nyengine kuchelewa kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nilishauri hapa kwamba wawakilishi wawasaidie wananchi wao kuhakikisha kwamba hizi fomu zinajazwa sawa sawa na michanganuo ya miradi inakuwa ndio ili zisipate mkwamo wowote. Kwa hivyo, ni juhudi zenu nyinyi Wawakilishi ndizo zitakazowasaidia wananchi wenu kuhakikisha. Sio tu mikopo hii, lakini mikopo iko mingi na Waheshimiwa Wawakilishi mchangamke kuwatafutia watu wenu mikopo.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la nyongeza alisema kwamba Waheshimiwa Wawakilishi wawasaidie kujaza fomu wananchi vizuri ili zisiharibike.

(a) Je, Mhe. Waziri tokea kuja utaratibu huo wa mfuko amewahi kuwaita wawakilishi angalau akawapiga semina ili wakajua wananchi wawafahamishe vipi?

(b) Fedha hizi zimeletwa kwa madhumuni ya kupunguza umaskini. Katika kipindi kilichopita ndani ya Baraza hili tulihoji sana na Mhe. Waziri Kiongozi akasema atachukua juhudi hasa Kaskazini kwenda na kuona kiwango kimefikia vipi, lakini mpaka leo halijatendeka. Je, Mhe. Waziri hizi pesa bado zipo au hazipo. Kama zipo nini kikwazo?

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, hali ya wizara yangu kifedha nimeshaisemea sana. Lakini kama ningekuwa nazo hizo fedha za kutosha basi ningefanya semina ili nikiondoka pale mjue nini mchango wenu katika kuharakisha kasi ya kupatikana hizi fedha.

Mhe. Mwenyekiti, la pili ni kwamba hizi fedha zipo na zinaendelea kukopeshwa.

Mhe. Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa fursa hii nina maelezo kidogo ya ziada. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Ame Mati Wadi kama alivyosema nilitoa ahadi kwamba nitakutana na viongozi wa Mkoa wa Kaskazini ili kutafakari na kujadili suala la upatikanaji wa fedha hizi zinazotokana na Mfuko wa

Uwezeshaji wa Wananchi zinazotokana na mchango huo wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Rais Amani Abeid Karume.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli nilitoa ahadi hiyo, lakini ahadi hiyo haikuwa ya hewa. Hivi karibuni nilikutana na waheshimiwa wabunge na waheshimiwa wawakilishi nikawaeleza juu ya dhamira hiyo ya kutekeleza agizo hilo. Wakanambia kwamba katika kipindi hiki ambacho mimi nimepanga kukutana nao wanasema wabunge hawatakuwepo wapo kwenye shughuli za Kamati na Bunge. Kwa maana hiyo, wanadhani isingekuwa vizuri nikazungumza na waheshimiwa wawakilishi tu peke yao, niwasubiri mpaka nao wakiwepo tuzungumze ili tupate mawazo ya jumla. Mimi sikuona kama wazo hilo ni baya.

Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu akitujaalia wakimaliza shughuli za Bunge na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutakuwa tumeshamaliza shughuli za Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, baada ya kumaliza shughuli hizo za Bunge basi nitatekeleza ahadi hiyo kama nilivyokwisha kuitoa hapa. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Nam. 60

Utoaji wa Mkopo wa Uwezeshaji Wananchi

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa.

Shughuli za Serikali

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar Nam. 8 ya 1999

(Kusomwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Marekebisho ya Sheria Nam. 8 ya 1999 ya Kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kwa Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, nia na azma ya warka huu ninaouwasilisha una lengo la kurekebisha tu kile kifungu ambacho kimekusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo kama nilivyosema madhumuni ya warka huu ambao nauwasilisha mapendekezo ya kurekebisha sehemu ya nne ambayo inaelezea masuala ya uongozi na utawala ikiwemo uteuzi wa viongozi mbali mbali,

uundwaji wa Baraza za Kamati za Chuo. Marekebisho pia yatafanywa katika sehemu nyengine zinazohusiana na uongozi na utawala.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo kina Mkuu wa Chuo *(Chancellor)* ambaye ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akisaidiwa na Makamo Mkuu wa Chuo ambaye anachaguliwa na Rais. Pia kutakuwa na Naibu Makamo Mkuu wa Chuo atakayechaguliwa na Rais, pamoja na Mrajis wa Chuo ambaye anachaguliwa na Baraza la Chuo.

Pamoja na ngazi hizo za uongozi, sheria imeainisha kuwepo kwa Baraza la Chuo, Kamati ya Ajira, Seneti na Kamati nyengine ambazo zitaundwa pale itakapoonekana ipo haja ya kufanya hivyo sehemu hii. Pia imeainisha kuwepo kwa skuli mbali mbali za chuo, bodi na idara zake.

Kutokana na kupanuka kwa chuo na kwa kuzingatia masharti ya Baraza la Vyuo Vikuu vya Tanzania, wizara imeona ipo haja ya kufanya marekebisho hayo ambayo nimeyaeleza hapo juu.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo wizara inapendekeza kufanywa marekebisho katika kifungu cha 10 ambacho kinaeleza kuwa “Kutakuwa na Naibu Makamo Mkuu wa Chuo ambaye atateuliwa na Baraza Kuu kutoka katika orodha ya Maprofesa wa Chuo Kikuu wasiozidi watano na wasiopungua wawili wenye uzoefu wa kiutawala. Orodha ya majina itawasilishwa kwa Kamati ya Uchunguzi ya Wajumbe Watatu iliyoundwa na Baraza Kuu baada ya Baraza Kuu kutakiwa kufanya hivyo na Makamo Mkuu wa Chuo.

Inapendekezwa kwamba kifungu hicho kifutwe na kirekebishwe kama ifuatavyo:

Kutakuwa na Manaibu Makamo Wakuu wa Chuo wawili wa Taaluma na Utawala watakaoteuliwa na Rais. Pia Rais anaweza kuteua Manaibu Makamo Wakuu wa Chuo wengine ikionekana ipo haja ya kufanya hivyo. Manaibu Makamo Wakuu wa Chuo wanaweza kuteuliwa miongoni mwa wafanyakazi wa chuo au nje ya chuo wenye sifa zinazokubalika na wenye uzoefu wa kazi ya kitaaluma na utawala kwa miaka saba katika chuo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 11 kinachozungumzia kuwepo kwa mrajisi na kazi zake kinafutwa kwa vile kazi zitafanywa na Naibu Makamo Mkuu wa Chuo anayeshughulikia utawala.

Katika kifungu cha 12 kinachozungumzia kuundwa kwa Baraza na wajumbe Naibu Makamo Mkuu anayeshughulikia utawala atakuwa Katibu wa Baraza.

Katika kifungu cha 16 kinachorekebishwa kuhusu kamati ya uteuzi ya wafanyakazi na nafasi ya mrajisi inachukuliwa na Naibu Makamo Mkuu wa Chuo Utawala ambaye anakua Makamo Mwenyekiti wa Kamati hiyo.
Kifungu cha 18 kuhusu kuwepo kwa *senate* ya chuo na wajumbe wake, nafasi ya mrajisi inachukuliwa na Naibu Mkuu wa Chuo Utawala na Naibu Makamo Mkuu wa Chuo Taaluma anakuwa Makamo Mwenyekiti wa *senate.*

Katika kifungu cha 23 kuhusu kada ya watumishi, wataalamu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma atakuwa kiongozi wa kada hii.

Katika kifungu cha 26 kinachohusu kada ya utawala Naibu Makamo Mkuu wa Chuo Utawala atakuwa kiongozi wa kada hii na nafasi ya Mrajisi inaondoka.

Kifungu cha 37 kuhusu kuwepo kwa mkusanyiko yaani *convocation* nafasi ya Mrajisi inachukuliwa na Naibu Makamo Mkuu wa Chuo Utawala.

Katika kifungu cha 40 na 41 neno "mrajisi" linafutwa na badala yake kuweka neno "Naibu Makamo Mkuu wa Chuo Utawala".

Marekebisho pia yanapendekeza katika jaduweli ya kwanza kifungu cha 11(2) kwa kufuta cheo cha mrajisi katika kipengele cha (c) na kuwa Naibu Mkuu wa Chuo katika kipengele cha (b) katika jaduweli la pili, vifungu vya kwanza na pili, cheo cha mrajisi pia kinafutwa na kuwekwa Naibu Makamo Mkuu wa Chuo.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho haya yanayopendekezwa yatakiwezesha Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kuwa na uwezo wa kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi na kwenda sambamba na taratibu za vyuo vikuu vingine hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ridhaa ya Baraza lako tukufu chini ya uongozi wako, kufanyiwa marekebisho yanayopendekezwa sheria hii ya kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar ya mwaka 1999. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe Ali Suleiman Ali: (Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa kabla sijatoa maoni ya hotuba ya kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii juu ya Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar nambari 8 ya mwaka 1999. Kwa heshima yako na kwa ruhusa yako naomba nitowe taarifa hii ifuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa hii kwa niaba ya wajumbe wote wa Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, juu ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kupata kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa nchi 15, zilizo Kusini na Mashariki ya Afrika, katika kuangalia ubora wa elimu. Hiyo ni fahari ya nchi yetu ya Zanzibar. Pia ni fahari ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya utawala bora, na mwelekeo mzuri ambao unastahiki kupata heshima hiyo. Kwa hivyo, kwa niaba ya kamati naomba kutoa taarifa hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mara nyengine tena kwa kutujaalia kuweza kukutana tukiwa na afya njema, ili kuendeleza shughuli za kawaida za Baraza lako tukufu.

Pili naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu ili kutoa maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii Juu ya Mswada wa Sheria ya kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar nam. 8 ya mwaka 1999.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, naomba nitoe Shukrani za dhati kwa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na watendaji wake kwa ushirikiano mzuri waliouonesha kwa kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mswada kwa kamati ili uweze kujadiliwa na kufanyiwa marekebisho baada ya wajumbe kuupitia.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda nichukuwe nafasi hii kuwashukuru wajumbe wenzangu wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa ushirikiano wao mzuri waliouonesha wakati tulipoupitia na kuujadili Mswada huu, Wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:-

1.	Mhe. Ali Suleiman Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Ame Mati Wadi	-	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Abubakary Kh. Bakari	-	Mjumbe
4.	Mhe. Ali Haji Ali	-	Mjumbe
5.	Mhe. Ali Mzee Ali	-	Mjumbe
6.	Mhe. Haji Faki Shaali	-	Mjumbe
7.	Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	-	Mjumbe
8.	Mhe. Muhammed Ali Salim	-	Mjumbe
9.	Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak	-	Mjumbe
10.	Mhe. Raya Suleiman Hamad	-	Mjumbe
11.	Mhe. Salim Abdalla Hamad	-	Mjumbe
12.	Ndg. Ramadhan Khamis Masoud	-	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Maendeleo ya Elimu ni sehemu muhimu sana katika uboreshaji wa maendeleo ya nchi yoyote duniani. Ndio maana nchi mbali mbali zimo katika jitihada za kukuza na kuendeleza elimu, ikiwa ni pamoja na kuboresha taasisi zao ambazo zina dhima ya utoaji wa elimu.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ikiwa ni sehemu ya dunia na sisi tuna haja na wajibu wa kuboresha elimu kwa kuzijengea uwezo mzuri taasisi ambazo zinahusika na utoaji wa elimu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na lengo la uboreshaji elimu mswada huu wa sheria ya kurekebisha sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar Namba 8 ya 1999, pia una lengo la kukifanya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) kwenda sambamba na kulingana na vyuo vyengine vya Tanzania .

Mhe. Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, ndicho chuo kikuu pekee ambacho kinamilikiwa na Serikali hapa Zanzibar, hivyo kuna kila sababu ya kuboresha ufanisi wake, ikiwa ni pamoja na kutunga sheria itakayotoa njia nzuri na urahisi kufikia ubora huo ili kiwe ni kigezo kizuri, kwa vyuo vyengine viliopo nchini ikiwa ni pamoja na kuijengea sifa nzuri nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umejaribu kurekebisha sehemu mbali mabali zinazo husu Chuo Kikuu, ikiwemo uongezwaji wa maneno, ubadilishaji wa baadhi ya maneno, ili kuweka maneno yatakayo leta tafsiri ya uwazi na yenye kufahamika zaidi na urekebishaji wa baadhi ya maneno ambayo yalitokana na makosa ya kiuchapaji, pia marekebisho mengine yanahusu ubadilishwaji wa nambari za vifungu, kutokana na kuongezwa kwa baadhi ya vifungu ambavyo havikuwepo hapo mwanzo kabla ya marekebisho haya.

Mhe. Mwenyekiti, katika Ukurasa wa 53 kifungu (1) kumeongezwa maneno “Cha Zanzibar” mbele ya neno “Taifa”, ili kuleta maana halisi ya Jina la Chuo, yaaani badala ya kusomeka chuo kikuu cha Taifa kisomeke Chuo Kikuu Cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*), marekebisho kama hayo yamefanyika katika ukurasa wa 54 kifungu cha (2).

Pia, kuna marekebisho ya maneno, ambapo baadhi ya maneno yalirekebishwa ili kuleta uwiano wa kisarufi katika hali ya umoja na wingi. Katika ukurasa huohuo wa 54 kifungu cha(2),neno **“**mkuu**”** limebadilishwa na kuwekwa katika hali ya wingi ili lisomeke **“**wakuu**”,** ili kifungu kisomeke “Manaibu wakuu wa chuo” badala ya **“**Manaibu Mkuu wa Chuo**”.**

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu wa sheria ya kurekebisha sheria ya Chuo Kikuu cha Zanzibar Nam. 8 ya 1999, vile vile umefanya marekebisho katika

muundo wa uongozi wa chuo pamoja na jinsi ya kuupata Viongozi wa Chuo hicho.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 10, 11 na 12 vya mswada vinavyohusu kifungu cha 37(2), 40(1) na (2) vya Sheria mama vinarekebishwa na kuwekwa maneno "Naibu Makamo Mkuu Taaluma**"** badala ya Neno "Mrajis**". M**abadiliko haya yanatokana na ubadilishwaji wa muundo wa uongozi ambapo badala ya kuwepo Naibu Makamo Mkuu wa Chuo, patakuwa na Manaibu Wakuu wawili na hapatokuwa na Mrajisi, Ili Kuleta Ufanisi na kupunguza Gharama za Uendeshaji.

Mhe. Mwenyekiti, hii itasaidia katika upatikanaji wa uongozi ulio bora zaidi, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha uwajibikaji kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ilikaa na kujadiliana kwa kina juu ya mswada huu, na kutoa maoni mbali mbali kwa kuufanyia marekebisho ya vifungu, napia kubadilisha baadhi ya maneno, kwa kuweka maneno ambayo yataleta tafsiri ya uwazi zaidi na ambayo yanafahamika kiurahisi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho, ningewaomba Wajumbe wenzangu waupitie mswada huu kwa makini ili na wao watowe michango yao na baadae kuupitisha, tukitumai kwamba kupita kwa mswada huu kutasaidia kuleta mabadiliko ya kiutendaji katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*).

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijawasilisha mbele yako hotuba hii, naomba na mimi nichangie kwa niaba ya jimbo langu.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukuwe fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wote, hasa tukizingatia sasa hivi umefika wakati kwamba Zanzibar kimaendeleo ya elimu imebadilika sana.

Mhe. Mwenyekiti, nina hakika hivi sasa hapa kwetu vijana wetu wengi wa kike na wa kiume wameongeza ari ya kupata elimu. Huko nyuma tunakotoka ilikuwa shida hiyo ipo kwa muda mrefu, lakini serikali baada ya kukaa, kutafakari na kuona kwamba kuna haja ya kuanzisha Chuo Kikuu, basi baada ya kuanzishwa vyuo vikuu hivi vijana wetu wengi wamefaidika.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa ukenda katika chuo cha *SUZA* na vyuo vyengine, lakini tunazungumzia zaidi *SUZA*, nafasi kupatikana inakuwa ni tabu na watu wanazigombea nafasi. Hiyo inaonesha dhahiri kwamba ufanisi wake ni bora na unaelekea katika mwelekeo ambao ni wa kuliletea taifa heshima na pia kuweka

taifa letu kwenye watu wenye elimu na kuendelea kwenye ukuaji wa pato la maisha na mambo mengine ambayo yanahitajika.

Kwa hivyo, mimi namshukuru sana Mhe. Waziri kwa hili na wakati huu ulioletwa mswada huu ni wakati mzuri kwa marekebisho haya, hasa tukizingatia kwamba kila ufanisi ukipatikana kuwa mzuri basi na vijana wetu wanajitokeza kwa wingi ili kuleta maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa siku ya leo kuwepo katika kiti chako hicho, naamini Mhe. Mwenyekiti, uendeshaji wako na hekima yako uliyokuwa nayo basi kila mmoja atapata nafasi nzuri ya kuchangia na kutoa maoni yake, ili kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri katika kuuchangia mswada huu na kupata faida.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati yangu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, na kwa niaba ya wananchi wangu wote wa Jimbo la Kwahani, tunaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.*(Makofi).*

Mhe. Muhammed Ali Salim: (Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, na mimi kabla sijasoma hotuba ya Waziri Kivuli, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali juu ya Maoni ya Kambi ya Upinzani, ya Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar nambari 8 ya mwaka 1999.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii adhimu kumpongeza Mhe. Waziri kwa nafasi mpya aliyoipata. Jambo ambalo limeleta utambuzi zaidi wa nchi yetu ya Zanzibar. Kwa sababu siku zote tulikuwa tunapiga kelele kuwa Zanzibar ni nchi. Pia tulikuwa tunapiga ke
lele kuwa kuna watu wanaitaka ifutike katika ramani ya dunia, lakini bado inaendelea na hii ndio ithibati moja, kuwa bado Zanzibar inaeleweka. *(Makofi).*

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nisome hotuba hii ya Maoni ya Kambi ya Upinzani, juu ya Marekebisho ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar nambari 8 ya mwaka 1999.

Mhe. Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Allah, Mola anayestahiki kushukuriwa kwa neema zake anazotupatia waja wake bila ya kujali kuwa tunamtii au la. Baada ya shukrani hizo kwa muumba wetu nakushukuru na wewe Mhe. mwenyekiti, kwa kuzifuata kanuni zinazoongoza Baraza hili na ukaniruhusu nitoe maoni haya ya Kambi ya Upinzani yanayohusu Mswada wa Sheria niliyoitaja hapo mwanzo.

Aidha, namshukuru Kiongozi wangu wa Kambi ya Upinzani Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwa kuniongoza vyema, na nikaweza kuandika hotuba hii fupi. Ninawaomba wajumbe wa Baraza lako hili la wananchi wanisikilize vizuri na wasichoke mpaka nimalize kusoma maoni haya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitangulize maelezo machache ya jumla juu ya mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ina mashaka na jinsi Miswada inavyoshughulikiwa, kuanzia kwenye Kamati na hata Barazani. Tunaelewa kuwa Mswada unaotiwa saini na Rais baada ya kupitishwa Barazani ni ule ulioandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Lakini wajumbe wako wa Kamati na hata wa Baraza mara nyingi hushughulikia zaidi na mwishowe huupitisha ule ulioandikwa kwa Kiswahili. Mswada wa Kiswahili ni tafsiri tu ya mswada wa Kiingereza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wafasiri wa miswada hiyo wana uwezo tafauti wa kazi hiyo mara nyingi kunakuwa na baadhi ya tafauti za msingi kati ya miswada hiyo miwili. Hata katika marekebisho yanayofanywa na Kamati na hata Baraza hurekebishwa ule wa Kiswahili na kuachwa kabisa ule wa kiingereza.

Je, Mhe. Mwenyekiti, hatuoni kuwa mswada tunaoupitisha na sheria inayopelekwa mahakamani ni vitu viwili vinavyotafautiana? Wakati mwengine hali hiyo inasababishwa na kucheleweshwa miswada ya Kiingereza kufikishwa kwa wajumbe, ingawa wakati mwengine na wajumbe wenyewe kutokuupa uzito mswada wa Kiingereza. Katika hili kuna haja ya kufanya marekebisho yanayofaa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye yanayohusu mswada wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu ni mfupi sana, lakini ni muhimu. Katika madhumuni na sababu za kuletwa mswada huu ni kukifanya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kilingane na vyuo vingine vilivyopo Tanzania. Hata hivyo si vyema kuangalia vyuo vya Tanzania tu bali tungepaswa kuangali hata nchi za nje ambazo zinafanana na sisi zinakwendaje, ili tuwe na upeo mkubwa zaidi katika kurekebisha mambo yetu, hasa kwa kuwa sheria ya vyuo vikuu vya Tanzania sisi haituhusu kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho hasa yaliyokusudiwa kufanywa katika sheria hii ni haya yafuatayo:-

a) Kuondoa cheo cha Mrajis
b) Kuondoa cheo cha Naibu Makamo Mkuu wa Chuo
c) Kuweka Naibu Makamo Mkuu wa Chuo Utawala na Naibu Makamo Mkuu wa Chuo Taaluma na kuweka nafasi ya kuwa na Naibu Makamo Mkuu wa Chuo mwengine pale inapohitajika.
d) Kuzigawa kazi za Mrajis na Naibu Makamo Mkuu wa Chuo walioondolewa kwa Manaibu Wakuu wa Chuo walioongezwa.

Kwa ufupi mabadiliko yanayofanywa yanahusu uongozi wa chuo.

Mhe. Mwenyekiti, Naibu Makamo Mkuu wa Chuo kwa mujibu wa sheria hii anashika madaraka kwa miaka mitatu na anaweza akaongezwa mitatu mingine, lakini sheria haikusema kama Naibu Makamo Mkuu wa Chuo Taaluma, kwa mfano baada ya kumaliza uteuzi wa mara mbili wa nafasi hiyo, jee ataweza kuteuliwa tena kuwa Naibu Mkuu wa Chuo utawala, sababu sio cheo alichokifanyia kazi. Kuna haja ya jambo hili kuwekwa wazi katika sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, uzoefu unatuonesha kuwa kuweka sheria ni kitu kimoja na utekelezaji wake ni kitu kingine tafauti. Kwani chuo hiki hiki sheria yake iliweka nafasi ya Naibu Mkuu wa Chuo tangu mwaka 1999 lakini ilikaa wazi muda mrefu mpaka tukahoji hapa Barazani ndio ikajazwa mwaka huu. Hivyo basi Kambi ya Upinzani inafanya hesabu rahisi ya kulinganisha na inauliza ikiwa Makamo Naibu Mkuu wa Chuo mmoja tu alichukua miaka kupatikana, jee sasa wawili watachukua muda gani? Hivyo basi Kambi ya Upinzani inaisihi Serikali ichukue hatua ya haraka ya kujaza nafasi hizo, mara mswada utakaopitishwa ukishakuwa sheria, kwani viongozi hao wana majukumu makubwa waliyopangiwa.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine muhimu sana ni kuwa na sheria inayotoa mwongozo wa vyuo vikuu vya Zanzibar, sasa hivi tunafanya mabadiliko haya ya uongozi wa *SUZA* kwa kujilinganisha na vyuo vya Tanzania. Tanzania wao wana sheria inayoongoza vyuo vyote vikuu, sisi hatuna na ile sheria yao sisi haituhusu. Kwa hivyo ni vyema tukawa na sheria yetu inayoongoza vyuo vikuu vya Zanzibar, ili tunapofanya marekebisho yafuate sheria hiyo. Lakini pia kuwapo kwa sheria hiyo kutafanya vyuo vikuu vya Zanzibar vyenyewe vifanane. Sheria hiyo hiyo itakuwa ndiyo sukani ya vyuo vikuu vya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, haitoshi kuimarisha uongozi wa Chuo Kikuu bila ya kuimarisha upatikanaji wa wasomaji wa chuo hicho. Hivi sasa tayari tunavyo vyuo vikuu vitatu hapa Zanzibar. Vyote hivi vinahitaji kupata wanafunzi wenye sifa ya kujiunga na vyuo hivyo. Sio vyuo vya Zanzibar tu vyenye haja ya kupata wanafunzi kutoka Zanzibar bali hata vyuo vya Tanzania navyo

huteka wanafunzi huku huku. Kambi ya Upinzani inahoji je, Serikali imejitayarishaje na upatikanaji wa wanafunzi hao?

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa uwiano wa waombaji wa vyuo vikuu hapa Zanzibar kwa aina ya masomo mbali mbali sio mzuri. Waombaji wengi ni wa masomo ya sanaa. Pamoja na kuhitaji watembeza watalii na mameneja wa mahoteli pia kuna haja kubwa huko huko kwenye mahoteli ya kupatikana mafundi wa mambo mbali mbali ili hoteli hizo ziweze kwenda vizuri. Kwa mfano mafundi wa umeme, mafundi wa magari, mafundi wa uchongaji na wengine, wote hao wanahitajika.

Mhe. Mwenyekiti, la hoteli ni dogo, lakini nchi yenyewe inahitaji wataalamu mbali mbali kwa maendeleo yake. Nchi inahitaji wanasayansi, mafundi mbali mbali na wanaoweza kucheza na mtandao vizuri yaani (*ICT*). Hao wote hawateremki tu kama mvua, bali wanahitaji matayarisho yakutosha. Wanafunzi wengi wanayakimbia masomo ya sayansi kutokana na mazingira mabovu ya kusomea masomo hayo. Kuna matatizo ya walimu ambapo katika skuli ukibahatika na mwalimu mmoja wa sayansi huwa umeokota lulu hasa skuli za vijijini. Pia kuna matatizo ya walimu wa ufundi, ukiachilia mbali walimu wa mambo ya kompyuta ambao nao ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa vifaa Mhe. Mwenyekiti, hapana asiyejua hali ya skuli zetu, vifaa vya sayansi na vya ufundi ni adimu sana. Hufikia hata mwanafunzi kasomea ufundi lakini akipasi hataki kuendelea na mafunzo ya ufundi kwa kuwa hakupata elimu ya vitendo katika skuli aliyosoma na huona hana la kwenda kufanya kwenye ufundi, kwani kusoma kwa nadharia unaweza ukajibu maswali ya nadharia, lakini hakuwezeshi kufanya vitendo. Ama kwa upande wa kompyuta ni skuli chache mno zilizobahatika na baadhi yao hazina walimu.

Mhe. Mwenyekiti, hali hii haifanyi mazingira mazuri ya kutayarisha wanafunzi wa kujiunga na vyuo vikuu vyetu. Ndio maana tukapata waombaji wengi sana wa mafunzo ya sanaa kuliko masomo mengine, jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo inafaa tuliangalie ni hali ya umasikini ya wananchi wa Zanzibar. Kutokana na hali hiyo, ili wanafunzi waweze kusoma ni lazima kuwe na mpango kabambe wa upatikanaji wa fedha kwa wanafunzi. Hivyo basi kuna haja ya serikali kujitayarisha vizuri kwa utoaji wa mikopo. Mpango wa kuchagua wakupewa mikopo na wengine kuachwa au mpango wa ucheleweshaji sana wa ulipaji katika vyuo kwa mfuko huo wa mikopo linarudisha nyuma ari ya wanafunzi ya kujifunza. Kwa mfano, inafika

wakati wanafunzi bado siku mbili tu kufanya mitihani lakini bado mfuko haujawalipia chuoni. Hali hiyo inawafanya wanafunzi wachanganyikiwe.

Mhe. Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaishauri serikali ijitahidi katika matayarisho ya wanafunzi wa kujiunga na vyuo vikuu. Kwa wale ambao tayari ni wanafunzi wa vyuo hivyo ili wasome bila ya hofu, serikali itakapotimiza wajibu wake ndipo wazee na wanafunzi watakapofanya majukumu yao ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kukushukuru kwa kunivumilia nikasoma hotuba hii bila ya kunikatisha. Aidha, naomba niwashukuru wajumbe wa Baraza hili kwa kunisikiliza kwa makini muda wote. Ni matumaini yetu kuwa waraka huu utakuwa kichecheo cha maendeleo ya elimu nchini kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Sina majina.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, huna majina, mimi jina langu Mhe. Haji Mkema Haji Mwakilishi wa Jimbo la Koani.

Nimesimama hapa Mhe. Mwenyekiti, kuunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, juu ya mswada huu wa marekebisho ya Sheria ya Uanzishwaji wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na tukaweza kufika kwenye kikao chako hiki, ili kujadili masuala yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pili na mimi niungane na Mhe. Mjumbe aliyeondoka, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mkoani, Mhe. Muhammed Ali Salim, kumpongeza Mhe. Waziri kwa dhati kabisa, kwa kuchaguliwa kwa nafasi yake mpya ya kuongoza Shirika hili la Elimu katika nchi kumi na saba (17) za Bara la Afrika, kuhusiana na shughuli za Kijumuiya ya Kimataifa. Kwa kweli hii haikumpa heshima yeye tu, lakini imeipa heshima Zanzibar na Tanzania kwa jumla *(Makofi)*.

Kwa hivyo, namuombea Mwenyezi Mungu amjaalie uzima na muda mrefu na afya nzuri, ili nafasi hii aliyoteuliwa aweze kuzifanya kazi zake kwa busara, hekima pamoja na ufanisi wa hali ya juu, kwa ajili ya kuleta sifa kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu nataka kuzungumza mambo machache. Kwanza nataka kuzungumzia kuhusu nafasi ya kuondoshwa Mrajis Mkuu. Kwa sababu Chuo Kikuu watumishi wake wanakuwa ni wataalamu wa fani mbali

mbali tena za hali ya juu na wala sio *degree* ya kwanza au ya pili ama ya tatu na hilo la kwanza.

Vile vile Vyuo Vikuu vinahitaji watu hawa au walimu wa aina hii kuwa wengi zaidi. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti hilo napenda Mhe. Waziri alifahamu na kuhakikisha ametuandalia mikakati mikubwa kabisa ya kuona tunapata walimu wa kutosha katika vyuo hivi.

Lakini nilisema nazungumzia nafasi ya Mrajis, kwa kweli anayo nafasi kubwa katika shughuli za uendeshaji wa chuo, mbali na kupendekezwa kuteuliwa manaibu Makamo Wakuu wa Chuo wawili, mmoja ambaye atashughulikia na utawala pia awe na shughuli za urajis.

Mhe. Mwenyekiti, hapa naona tunamuongezea mzigo mkubwa. Kwa sababu kwa nafasi zote hizo kuanzia Makamo Mkuu, Manaibu wote baadhi ya wakati kwa mujibu wa shughuli zao wanapata au wapewe nafasi kutoa elimu yao kwa wanafunzi, yaani wachukue vipindi kwenye madarasa.

Sasa leo Makamo Mkuu wa Chuo au Naibu Makamo Mkuu wa Chuo ukimpa shughuli zake za utawala na halafu shughuli kubwa nzito katika chuo suala la urajis ni shughuli kubwa unampa na hizo, nadhani hali hii inamnyima nafasi ya kupata muda wa kwenda kusomesha.

Kwa hivyo, mtu anapokosa nafasi ya kwenda kusomesha kwanza uzoefu au elimu yake inadumaa. Vile vile ule ujuzi wake ambao pengine serikali imechukua nafasi kubwa kwa ajili ya kusomesha wanafunzi wetu au nchi inaukosa, kutokana na kufanyakazi za kiutawala na zile za urajis. Mhe. Mwenyekiti, bado nafasi ya urajis ningependelea iwepo *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa tunafanya hivi kwa upungufu wa wanafunzi, basi ile nafasi bora iwe kwamba atafanya kazi za utawala na urajis, lakini nafasi ya urajis kuondoshwa moja kwa moja sikubaliani nalo kwa maoni yangu. Kwa hivyo, ni vyema nafasi hii ikawepo, labda tuseme tu kwa kuwa tunao upungufu, basi huyu Naibu Makamo Mkuu wa Chuo ambaye atashughulikia na utawala afanye kazi za urajis kutoka na mapungufu.

Lakini katika Chuo Kikuu nafasi hizi mbili zina nafasi kubwa tena nzito, kuweza kuzifanya mtu kwa pamoja. Sasa sijui wenyewe kwenye kamati ya Kitaalamu, lakini kwa maoni yangu naona nafasi hii bado iendelee kuwepo, hata kama itafanywa na Makamo Mkuu, nafasi ile ipo na tutakapokuwa na watu wa kutosha, basi awepo Mrajis wa Chuo.

Nikiendela na mchango wangu kuna kifungu chengine kinachompa Naibu Makamo kuwa Katibu wa Baraza, suala hili nalikubali, lakini je akiwa hayupo? Kwa hivyo, nadhani pawe na kipengele yule Makamo mwengine achukue nafasi ile sio kuwa wazi au kuchaguliwa mtu mwengine, kama nafasi hii inastahiki kwa sifa za Naibu Makamo Mkuu wa Chuo kuwa ni Katibu wa Baraza.

Hivyo, ni vyema kama yule Nam. 1 hayupo, Nam. 2 achukue nafasi ya Katibu kwa muda ule atakapokuwa hayupo nchini au anaumwa ama kwa dharura nyengine yoyote ile labda amepata kazi za kiserikali, basi yule Makamo wa Pili aweze kuchukua nafasi hiyo *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, maeneo mengine kwa sababu nataka kuzungumzia kwa ujumla kuhusu masuala ya Chuo Kikuu. Kwa kweli hivi Vyuo Vikuu vimepewa fursa nyengine kwenye sheria mbali mbali kuwa na Serikali ya Wanafunzi. Katika serikali hizo mnakuwa na marais, waziri viongozi, washika fedha pamoja na mambo mengine kama hayo.

Kwa hivyo, katika hili naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwenye uendeshaji wa Vyuo vyetu Vikuu na sisi tukatizama kutokana na silka pamoja na maadili yetu. Kwa kweli tumezoea kusikia Vyuo Vikuu mbali mbali shughuli za usomeshaji haziendi vizuri, na hutokea vurugu ambazo husababishwa na wanafunzi. Ina maana kwenye Chuo Kikuu tunakuwa na uongozi wa aina mbili, yaani wanafunzi wanalo eneo lao na serikali kwa upande wake inakuwa na uongozi wake na hili linaleta matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwamba hivi sasa tuangalie utaratibu au kanuni zinazowapa uwezo Serikali za Wanafunzi, kama tunaiga nchi za nje. Kwa mfano, tunaona Kenya kila mwaka Chuo au Vyuo Vikuu vinafungwa miezi mitatu au minne, yaani wamepewa uhuru mkubwa sana kuweza kuvuruga mwenendo mzima wa shughuli za usomeshaji na utoaji wa taaluma katika Vyuo vyetu Vikuu na hapa bado hayajatokea. Lakini tumuombe Mwenyezi Mungu yasitokee hayo.

Pamoja na hayo katika Chuo Kikuu cha Tunguu iliwahi kutokea suala kama hilo, kwa bahati nzuri kwa busara za Mhe. Waziri alikwenda na kuweza kulizima tatizo lile. Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba baadhi ya Serikali za Wanafunzi katika Vyuo Vikuu vingi huanza kuleta matatizo na kuwaweka kiti moto Uongozi wa Chuo. Kwa hivyo, suala hili Mhe. Waziri alifahamu vizuri.

Suala jengine ambalo nadhani lingekuwemo huku kuhusu kuwasaidia wanafunzi wetu. Kwa sababu hivi sasa Sera yetu ya Elimu ni Kuchangia na

tumeipitisha hapa, katika hiyo imewekwa njia ya kuwasaidia kupitia mikopo, kuna mifuko ya mikopo kwa Tanzania nzima na pia sisi Zanzibar tumeona tujiwekee mfuko wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kuuliza katika ule Mfuko wa Jumla wa Tanzania nzima ni *percentage* ngapi ambayo tumewawekea wanafunzi wetu wa Zanzibar au ni mpata mpatae tu? Kwa sababu wenzetu ndio waliokaribu na siku zote aliyekaribu ndiye anayeanza kuangukiwa na mti. Kwa hivyo, ni kiasi gani ambacho tumeweza kuekewa katika mfuko huo, ili na sisi wanaotaka kwenda huko au kwenye vyuo vyetu vya hapa Zanzibar waweze kunufaika na mfuko huo?

Pili katika Mfuko wetu wa Zanzibar ni kwa kiasi gani mfuko huu umeendelea kutuna, ili na sisi wanafunzi wetu wa wakulima wa mwani, wavuvi pamoja wafugaji waweze kupata kwa ajili ya kujiendeleza. Kwa sababu kama alivyouliza hapa Mhe. Ali Suleiman Ali Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, kwamba hivi sasa kuna changamoto kubwa na wananchi wetu wamehamasika katika suala zima la kupata elimu ya juu.

Kwa kweli tulizoea hapo nyuma mtu akifika darasa la nne ameshatosheka, ikaja mtu akeshafika darasa la sita Dole msomi mkubwa, ikaja mtu akifika darasa la nane Beit-el- Raas msomi mkubwa. Baadaye kidogo kunako miaka ya 1947 mpaka 1947 mtu afike Makerere. Tulikuwa tukiambiwa mwanangu some mpaka ufike Makalele, yaani wanakusudia Makerere upate kuwa daktari. Lakini sasa tumetoka na Makerere na tuko na *SUZA*, kwa kweli tumepiga hatua kubwa.

Sasa ili twende huko basi tuhakikishe hawa tunaotaka kuwajenga mazingira haya ya Makamo Mkuu wa Chuo na Mrajis lazima wawepo kama hawapo hawa wanafunzi Makamo Mkuu wa Chuo atafanya nini au *SUZA* watafanya nini?

Kwa hivyo, ni vyema kuhakikisha kwamba hawa wanafunzi tunaotaka wapate elimu hii basi tunawaekea mazingira katika hali hii. Kwa sababu tumezungumza kwamba kuna kuchangia na wala sio wote wanaoweza kuchangia, lakini kuwepo kwa fursa hii basi tuone namna gani fursa hii inapatikana kwa wale watu wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo Kikuu kinatoa elimu ya juu na hii ni moja miongoni mwa mambo ya Muungano. Kwa kweli nasikitika sana kusema kwa miaka yote wenzetu wa Jamhuri ya Muungano hawajaona angalau kuweka kitengo au kitivo kimoja cha Chuo Kikuu hapa Zanzibar. Kwa sababu sisi wenyewe ni binadam tena tunazo akili basi tumeweza kujifikiria.

Kwa hivyo, naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya wazo hilo na tuendelee. Katika azma hii ya kuanzisha hapa, kwa sababu jambo hili ni la Muungano tena tunayo haki, tumewaambia kwa kiasi gani angalau waweze kusaidia na sisi tunaanza Masuala ya *Science* pamoja na *Engineering*, lakini tunataka mambo ya kilimo, je tumewaambia angala Kitivo cha Kilimo tuongeze? Kwa sababu na sisi ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Waziri amechukua hatua hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, lazima nisikitike kwa jambo hili la Muungano mpaka hivi sasa tuko nyuma juu ya hilo kutokana na Serikali ya Muungano kutupana. Kwa sababu wao hivi sasa wameshafikilia zaidi ya Vyuo Vikuu sita vya Taifa, yaani tayari wameshajenga pale kama Vile Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam (Mlimani), Chuo cha Afya cha Muhimbili (*MUHAS*), Chuo cha Ardhi na Maji Mwenge, Chuo cha Sokoine, Chuo cha Mzumbe, Mwanza Chuo cha *SAUT*, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Lakini bado sehemu hii ya pili ya Jamhuri mpaka hivi sasa hawajafikiri na hili ni jambo la kusikitisha sana na kweli Wazanzibari tunao wajibu wa kusikitika tena tunayo haki ya kusikitika, kwa sababu wanatuonea, yaani wanatunyima haki ambazo tumekubaliana kuwa zetu ziwe na Muungano na Vyuo Vikuu vyote wanajijengea wao sijui kwa misingi gani? Mhe. Mwenyekiti, suala la kutunyima Vyuo Vikuu au kutusaidia wenzetu wa Muungano tunasema ni kero kwetu na wasikie.

Kwa hivyo, nachukua nafasi hii kwenye kiriri kuwaambia wenzetu wa Tanzania Bara, wanatufanyia kero kutunyima haki katika elimu ya juu, bila ya kutuzingatia na sisi kutujenga chuo katika visiwa vyetu *(Makofi)*.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tunayo matatizo katika Walimu wa *Science*. Lakini nafahamu wakati kwenye vikao vyetu vya Chama Tawala, Rais wetu ambaye anakuwa ndiye Mwenyekiti wa Chama alitoa tamko, kuhakikisha kwamba kuanzia mwaka ule wanafunzi wote ambao watachukua masomo ya Sayansi katika fani ya ualimu na udaktari hawa watalipiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano moja kwa moja.

Kwa hivyo, naomba nimuulize Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, katika hatua hii tamko lile kwa upande wetu wa Zanzibar, na huyu ni Rais wa sehemu zote mbili za Jamhuri, na sisi ni sehemu ya Jamhuri. Kwa maana hiyo, limetekelezwa kwa kiasi gani kuona wanafunzi wanaochukua taaluma ya ualimu, masuala ya *Engineering*, udaktari, yaani wamepewa fursa ya kauli ya Mhe. Rais?, Au bado wanaingia kwenye mchakato wa mkopo? Mhe.

Mwenyekiti, naomba hapa anisaidie kwa ajili ya kuweza kuboresha masuala yetu ya elimu.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri kwa sababu hivi sasa mambo yote yameshatimia ya kifedha pamoja na mazingira, basi achukue hatua ya kuharakisha mjenzi wetu kule kile Chuo chetu cha *SUZA* kule Tunguu, ambacho kiko katika Jimbo la Koani kimalizwe haraka, ili wanafunzi wetu waweze kusoma katika mazingira mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, wazo hili la kujenga pale limekuja kutokana na nafasi nyifu iliopo hapa Mnazimmoja, kweli tumeibana au tumeifisha Taasisi yetu ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, yaani uwezo wao wa kuchukua wanafunzi pamoja na kujipanua umeathirika kiasi fulani kutokana na kuingiziwa mzigo mwengine wa Chuo Kikuu cha *SUZA* katika sehemu ile.

Kwa hivyo, nasema hili makusudi iwe changamoto tuisaidie. Taasisi yetu ya Kiswahili na Lugha za Kigeni iweze kupanuka. Kwa sababu hizo lugha tunazozisikia zinazungumzwa mitaani, angalau waandishi wa habari waweze kusomeshwa pale, ili lugha yetu iweze kukua pamoja na kutumika vizuri katika vyombo vyetu mbali mbali vya habari kwa ajili ya kutoa taaluma vikiwemo redio, magazeti pamoja na televisheni.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya Waheshimiwa wangu ambao ndio wapiga kura wa Jimbo la Koani naunga mkono hoja hii *(Makofi)*.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kutoa mchango wangu mdogo tu kama mswada wenye ulivyo, yaani mdogo.

Kwanza nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kusini Unguja kumpongeza Mhe. Waziri kwa kupata nafasi ya kuwa Mwenyekiti wa nchi hizo 17 kama alivyosema Mhe. Haji Mkema Haji na tunamuombe dua aweze kufanya vizuri na kupata nafasi kubwa zaidi *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, mwanzo wowote mgumu. Kwa sababu nakumbuka wakati tunataka kuanzisha Chuo Kikuu Zanzibar na kwa kuwa kwenye Katiba ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania Masuala ya Elimu ya Juu ni ya Muungano, basi kidogo kulikuwa na matatizo. Lakini hatimaye kwa busara zilizotumika Zanzibar tumeweza kuwa na Chuo Kikuu cha Taifa.

Kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) kimetupa faraja ya kuona kwamba, sasa tutakuwa na wataalamu wa kutosha katika nchi yetu, ambao watakuwa wamepata elimu katika Chuo Kikuu chetu hicho. Kwa kweli elimu ni muhimu tena ndiyo yenyewe kusaidia nchi nyingi kupata maendeleo ya haraka, lakini elimu ikizidi nayo inaleta matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa niliyonayo kwamba India wako wasomi wa Vyuo Vikuu, lakini hawajapata kazi na hivi sasa wanafanyakazi za kuzoa taka, lakini na Japan nasikia nako vile vile. kwa hivyo, kazi ni kazi tu, lakini unapokuwa na elimu ni elimu kweli.

Sasa nije kwenye mswada wenyewe. Mswada huu ni mswada ambao unarekebisha kifungu cha 2, 10, 11, 12, 16, 18, 26, 37, 40 na 41. Lakini yote haya ni katika kutafuta njia ya kuweka Wakuu, yaani Makamo Wakuu wa Chuo. Kwa hivyo, katika kuweke Makamo wa Chuo hawakuekewa sifa gani wawe nazo, bila ya shaka lazima watakuwa ni wasomi. Katika usomi nadhani kuna haja ya kuongeza kitu hekima, busara, pamoja na ukereketwa wa maendeleo na sio wa chama.

Mhe. Mwenyekiti, hekima, busara pamoja na ukereketwa wa maendeleo katika sifa unasaidia sana. Kwa mfano, mimi mwenyewe sio Mkutubi na wala mtu ninayeshughulika na mambo ya *Library*, lakini Mhe. Rais alinitangaza kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Maktaba, basi mimi mwenyewe nilijiuliza, masuala ya Maktaba si yangu imekuwaje nikapewa nafasi hii?

Kwa hivyo, siku niliyokutana na Mhe. Rais aliniambia nimekupa nafasi nyengine unajua kwa nini? Nilimwambia sijui. Basi aliniambia kuna Maktaba inajengwa pale ambayo imeanza kujengwa tokea mwaka 1985 mpaka leo haijamaliza. Sasa fanya mipango ya yote uimalize ile Maktaba ndio maana nimekupa nafasi hii, najua mambo haya wewe si yako, lakini nataka unimalizie ile Maktaba kujengwa *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru na Mhe. Waziri alinichagulia Wajumbe wa Bodi ambao ni wazuri, baada ya kuzinduliwa tu kikao cha mwanzo tulichofanya tulikuwa tunazungumzia namna ya kumaliza ujenzi wa Maktaba. Namshukuru Mhe. Ali Suleiman Ali pamoja na Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi ambao ni wajumbe wangu wa bodi, tuliweza kusimamia hiyo kazi *(Makofi)*.

Kwa kweli fedha hatuna na tulianza kuomba omba na hatimaye Ubalozi wa *Japan* walikubali na kutusaidia. Maktaba tumemaliza japo kuwa hatujaifungua rasmi, lakini tumeshaifungua na watu wanasoma. Sasa tumo kwenye mipango ya kuifungua rasmi *(Makofi)*.

Lakini hatujaishia hapo tu, isipokuwa tumeomba na vitabu, na tumepata kutoka sehemu mbali mbali na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa sababu naye ni mjumbe wetu. Hivi sasa hicho Chuo Kikuu basi vitabu vyengine tunatoa Maktaba kuwapa wao pale.

Vile vile tunao utaratibu katika hizi *Teachers Training Centre* nao kuwapa vitabu, lengo letu mpaka skuli zote zinakuwa na *Library* na kuwapa vitabu, isipokuwa tunakwenda hatua kwa hatua.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa Pemba tayari tumeshapata eneo ambalo limeshapimwa na fedha zimehatolewa kwa ajili ya kupatiwa Hati Miliki, lakini kwa bahati mbaya eneo limekuwa dogo. Sasa juzi tumewapeleka wataalamu wetu kutoka wizarani kwa lengo la kuangalia eneo jengine. Kwa sababu tunataka na kule kujenga Maktaba kubwa kama tulivyojenga hapa.

Kwa hivyo, hizo ndizo busara, hekima pamoja na ukereketwa wa maendeleo. Sasa nadhani kwenye sifa basi hizo ziangaliwe zinaweza kutusaidia katika kukuza elimu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mswada huu ni mdogo, ambao unakurasa mbili tu. Kwa kweli cha kuchangia humu hamna, isipokuwa tusimame na tumpe ridhaa Mhe. Waziri ya kuweza kupata hawa Makamo Wakuu wa Chuo, kwa ajili ya kuendeleza elimu Zanzibar *(Makofi)*.

Kwa hayo machache nakushukuru kwa kunipa nafasi hii Mhe. Mwenyekiti na naunga mkono hoja hii.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia kuwa wazima na kuweza kuhudhuria katika kikao hiki cha Baraza, kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nami niungane na wale ambao wametangulia niwe miongoni mwa wachangiaji wa Marekebisho ya Mswada huu wa Sheria ya Chuo Kikuu cha Zanzibar (*SUZA*).

Kwanza nataka nikubaliane na marekebisho yote ambayo yamefanywa katika waraka huu uliotolewa. Isipokuwa kwenye marekebisho haya ninapengekezo katika eneo moja. Mhe. Mwenyekiti, pendekezo langu katika marekebisho ya

mswada huu ni pale ambapo umetajwa uteuzi wa Manaibu Makamo Wakuu wa Vyuo.

Kwa sababu hapa imetajwa kwamba watateuliwa miongoni mwa *Professors* wasiodizi watano na wasiopunguwa wawili, lakini wanaoteuliwa Mhe. Mwenyekiti ni wawili. Kwa hivyo, kama tunahitaji kupata uteuzi, maana yake hapa lazima tuwe na watu ambao katika wale wasiopunguwa watatu, kwa sababu wanaweza kuomba wawili na ikiwa hatupati ule uchaguzi wa kuteua wale ambao wanaotaka kuteuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba wafanye marekebisho hayo katika uteuzi wa watu wawili ambao wanataka kuteuliwa, basi *Professors* wasiozidi watano na katika kupunguwa wasiopunguwa watatu badala ya wawili. Kwa sababu tukisema wawili wanaweza kujaza wawili, na ikawa ndiye yale ambayo yapo, vile vile yawekwe masharti ya kwamba wasiopungua watatu.

Pamoja na hayo napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendani wote kwa jumla kwa juhudi kubwa walizozifanya, katika kuona umuhimu wa marekebisho haya ambayo yameletwa mbele yetu, yenye lengo la kuboresha zaidi Chuo chetu hiki Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*).

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa juhudi zake anazozifanya siku hadi siku, ili kuonesha kwamba maendeleo ya elimu kuanzia *Nursery*, *Primary*, *Secondary* mpaka *University*.

Kwa hiyo, naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa juhudi zake za dhati kabisa katika mbio zake zote anazokimbia, hasa tukizingatia juzi tu ametokea Ufaransa kwenye Makao Makuu ya Shirika la Kimataifa linaloshughulikia Masuala ya Elimu Duniani (*UNESCO*), ambako amepata nafasi ya uteuzi wa Mwenyekiti na kutuwakilisha na kuiweka Ramani ya Zanzibar kutambulika katika dunia *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, sikubaliani kabisa na mawazo ya Mhe. Mohamed Ali Salim (Waziri Kivuli Elimu na Mafunzo ya Amali) pale aliposema kwamba pengine hakuna juhudi ambazo zimechukuliwa na Wizara katika kuhakikisha kuwa wale ambao wamekwenda vyuoni na baada ya kutoka Chuo anakuwa hana cha kufanya, kwa sababu hakuna mambo aliyokuwa akiyafanya kwa vitendo.

Mhe. Mwenyekiti, hivi juzi tu Mhe. Rais wa Zanzibar pamoja na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, walikuwa pamoja katika ufunguzi wa Vyuo vya Amali Viwili hapa Zanzibar, yaani Chuo cha Amali cha Mkokotoni pamoja

na kile Chuo cha Amali cha Vitongoji Pemba. Kwa kweli Pemba sikwenda, lakini Mkokotoni nilikuwepo *(Makofi)*.

Katika vyuo vile kuna vifaa vingi ambavyo vimo ndani ya vyuo vile. Pia wenzetu ambao wale waliotusaidia *ADB* wamesema katika maeneo ambayo wameekeza Afrika Mashariki na Kati, basi Zanzibar ndio wamewekeza zaidi katika vyuo hivi viwili, kwa maana ya kwamba ni vyuo bora zaidi. Unaposema hakuna kitu ambacho kimeonesha maendeleo katika masuala ya elimu mimi sikuelewi. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali amesema wale watakaotoka chuoni watapewa vifaa vya kujiendeleza huko nje wanakokwenda, pamoja na fedha za kuanzia hizo kazi watakazokwenda kuzifanya baada ya kupata taaluma hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri Kivuli yeye anasema mtu akitoka hapo anashindwa kufanya lolote kwa sababu hakuna kitu ambacho amejifunza pale kwa masomo ya vitendo. Mimi sikubaliani nae na baada ya vile vifaa vya ufundi, pia mambo ya sayansi yapo pale, kompyuta pia wanasoma. Kwa kweli juhudi zipo na zinaonekana. Kwa hivyo, katika hili, naomba tutoe pongezi za makusudi kwa wizara pamoja na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mhe. Waziri wa Elimu ambaye anafanya kazi sambamba katika suala zima la elimu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nilikuwa nataka kulichangia katika marekebisho haya ni kwamba, kumetajwa suala la nidhamu. Mhe. Mwenyekiti, nidhamu katika chuo au mahala popote pale ambapo panaishi watu wengi basi ni jambo muhimu sana. Kwa hivyo, mimi napongeza sana hatua hii ya kuonesha kwamba, katika jambo ambalo limetiliwa mkazo ni kuwepo kwa nidhamu katika vyuo ambavyo vitaanzishwa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwape mfano mdogo ambao unaweza kuonesha athari ya kutokuwepo kwa nidhamu. Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa sababu ni mpenzi sana wa mpira wa miguu basi mara nyingi hutoa mifano katika zile sheria za mipira.

Mhe. Mwenyekiti, katika mpira wa miguu mnapocheza mechi, inakuwa kuna timu mbili zinazocheza na badala yake hapo kukafanyika fujo uwanjani, na fujo zitakazofanywa pale zinaweza kuanzishwa na mpenzi wa timu moja. Kwa hivyo, hapo inaweza mechi kuvinjika, ile timu ambayo imesababisha tatizo hilo inapoteza ushindi pamoja na faini, kuonesha uzito wa nidhamu katika mahala popote pale ambapo pana mkusanyiko wa watu. Kwa hivyo, suala la nidhamu nalipongeza kwa upande wa marekebisho haya kwamba lifanyiwe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu kwamba mswada huu sio mkubwa sana na mimi nilitaka nitoe baraka zangu katika hilo. Mhe.

Mwenyekiti, mimi mwenyewe na wananchi wangu wa Jimbo la Chaani tunaunga mkono marekebisho haya kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuja kutoa maelezo ya hapa na pale kidogo tu kwa sababu mswada wenyewe ni mfupi. Kwanza kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali naomba nipongeze sana wachangiaji wote ambao wamechangia leo.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wachangiaji waliochangi mswada huu ni 5, nao ni:-

1. Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati)
2. Mhe. Moh'd Ali Salim (Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu)
3. Mhe. Haji Mkema Haji
4. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja
5. Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nipongeze sana wale wote ambao wamechangia, na tumepokea pongezi zile ambazo wametupa. Mhe. Mwenyekiti, Mwenyekiti alizungumzia kwa ujumla juu ya marekebisho haya ambayo yamefanyika hapa, na ameyaunga mkono na hakukua na lolote lile ambalo alitaka turekebishe zaidi yale ambayo kamati ilipendekeza.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri Kivuli kwa pongezi zake tumezipokea na *inshaallah* tutaendelea kushirikiana zaidi katika maendeleo ya nchi yetu. Aidha, suala lake la mswada tunaoupitisha wa Kiswahili kwa Kiengereza hili kidogo ni la kisheria, lakini tumejitahidi sana kutafsiri kwa uhakika sana tumeona kwamba hakuna tofauti kubwa. Lakini hata hivyo tutakuwa makini zaidi kuliangalia suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii amesema ina utata kidogo katika mambo ya uteuzi, na alikuwa na mashaka pale kwenye Naibu Makamo Mkuu wa Chuo, uteuzi wake akishateuliwa mara ya pili kama atateuliwa tena. Sheria imesema pale anaweza akateuliwa kwa kipindi kingine. Kwa hivyo, tukihisi anafaa na Rais akiona kama anafaa kwa sababu yeye ndiye anayeteuwa basi anaweza akateuliwa tena, kwani haja yetu kuwa na watu ambao wana uzoefu na *experience* kubwa sana. Ndio maana yake hapa katika uteuzi wa Naibu Makamo Mkuu wa Chuo tumeweka miaka 7. Kwa hivyo, nafikiri itatosheleza kuteuwa tena mara nyengine kutokana na uwezo wake na akionekana anafaa, lakini tukiona amechoka inakuwa basi.

Mhe. Mwenyekiti, hapa limezungumzwa sana suala la kisheria, kwamba tuwe na sheria zetu hapa Zanzibar. Ni kwamba sheria ya Chuo Kikuu cha *SUZA* tunayo na ili kuifanya iwe ni bora zaidi na ilingane na hizo sheria nyengine za hapa Tanzania ndio tumeleta mabadiliko haya. Kwa sababu sheria ya awali ilikuwa inapendekeza kuwa na Naibu Makamo Mkuu wa Chuo mmoja na Mrajis, lakini tukaona ipo haja ya kukibadilisha.

Baadhi ya Vyuo Vikuu nje ya Tanzania kuna Makamo wa Vyuo Vikuu wanne, na kuendelea kutokana na haja ilivyo. Kwa hivyo, hapa ndio tumempa nafasi Mhe. Rais kama sheria ilivyompa nafasi, anaweza akateuwa wawili, au zaidi ya hapo akihisi kwamba inafaa. Mhe. Mwenyekiti, la msingi ni zaidi kwamba bado tunaendelea kuifuata sheria yetu ya *SUZA* ambayo imepitishwa na Baraza la Wawakilishi na tutaendelea kuitumia kwa sababu ndio sheria ambayo imepitishwa.

Mhe. Mwenyekiti, aidha nimesikia *concern* za Mhe. Mulla kuhusu *shortage* ya walimu wa sayansi.Tunakubali kwamba kweli kuna upungufu wa walimu wa sayansi, pia vifaa vya maktaba tuna upungufu navyo. Lakini ndio hizi juhudi ambazo zimefanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutafuta wahisani na washirika wetu wa maendeleo kusaidia katika maeneo hayo. Kwa hivyo, bado nalirejea tena suala lile lile kwamba, juhudi zinafanyika na *inshaallah* haitokuwa shida ya maisha hii, karibu tutaimaliza kwa sababu tumeshafika mahali pazuri.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mulla amezungumzia kuhusu mikopo kwa urefu, na nataka nimuhakikishie kwamba hali ya utoaji wa mikopo ni nzuri na tunafaidika kotekote kwenye SMT tunafaidika, na hapa Zanzibar tunafaidika. Hapa Zanzibar tumeongeza sana bajeti yetu ya mikopo, mwaka 2005-2006 tulikuwa tunapata *1.4 billion*, 2006-2007 tukawa tunapata 1.9 billion, 2007-2008 tulikuwa tunapata karibu *2 billion* na katika bajeti ya mwaka huu imeongezeka zaidi ya kiwango ambacho tumekuwa tukipata huko nyuma, tuko katika *2.3 billion.*

he. Mwenyekiti, yote haya ni kuhakikisha vijana wetu wenye sifa za kuingia vyuo vikuu tunawapa nafasi, na karibu wengi tumewapa nafasi karibu asilimia zaidi ya 95 walioomba nafasi tumewapa. Bado kuna malalamiko ya hapa na pale ambayo tunayafanyia kazi na yanapokuja tunajitahidi kuyatatua. Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi kumshukuru sana Mkurugenzi wa Elimu ya Juu kwa mashirikiano anayowapa wasomi hawa ambao wanataka kujiendeleza zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Haji Mkema Haji nae amepongeza, na amependekeza kwamba suala la Mrajis lingefaa tukalirejesha kwa sababu tusimpe kazi nyingi

huyu Naibu Makamo Mkuu wa Chuo, kwa sababu yeye atakuwa anasomesha na huku anafanya shughuli nyengine. Mimi nimefikiria hapa Mhe. Haji angepongeza kwa sababu huyo Mrajis tumempandisha cheo, sasa hivi badala yake anakuwa ni Naibu Makamo Mkuu wa Chuo anayehusika na mambo ya utawala. Tumefanya hivyo makusudi ili kumpa hadhi zaidi, na vyuo vikuu vingi masuala kama haya ya urajis yanapitwa na wakati kwa sababu ni *duplication* ya kazi ambazo zinafanywa.

Mhe. Mwenyekiti, ukitizama hata pale Wizara ya Elimu kulikuwa na Naibu Katibu Mkuu Taaluma, halafu tunae Kamishna wa Elimu. Kwa hivyo, tulihisi kwamba kuna *duplication* kwa hivyo Mhe. Rais alipofanya mabadiliko ya Makatibu wa Wakuu, Naibu Katibu Mkuu wetu wa Mipango Bi Mwanaidi sasa amekuwa Katibu Mkuu kamili. Kwa hivyo, hatukuweza kuchagua Naibu Katibu Mkuu anayehusika na taaluma, yule yule Naibu Katibu Mkuu mmoja anafanya kazi zote mbili, kwa sababu Kamishna yupo. Mhe. Mwenyekiti, tumejaribu kufanya hivyo na ndio maana huku *SUZA* tukafanya hivyo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile amependekeza suala zima la mikopo. Napenda nimuhakikishie Mhe. Haji kwamba tunafaidika na mikopo, SMT tumepata mikopo kwa wale ambao wamechukua mikopo. Taratibu zilizotolewa kule katika mfuko wa elimu ya juu kwamba wanaopata daraja la kwanza basi wote wanapata mikopo. Lakini safari hii kutokana na ufinyu wa bajeti ya SMT ilibidi baadhi ya wanafunzi ambao wanatoka Zanzibar wa mafunzo ya ualimu, basi walikosa mikopo hiyo, lakini walipokosa SMZ ikachuku hatua ya kuziba pengo hilo na tumeweza kuwalipia wote. Kama wapo ambao wana malalamiko basi waje tu na *inshaallah* serikali itafanya kila juhudi ili kuweza kuwalipia.

Mhe. Mwenyekiti, pia alizungumza suala la ujenzi wa Chuo Kikuu, lakini ni vizuri tukamueleza ujenzi wa Chuo Kikuu unaendelea vizuri mpaka sasa hivi. Ahadi yetu na Mkandarasi ni kwamba mwezi wa Mei atakabidhi chuo, nadhani kama amekwenda siku za hivi karibuni ataona juhudi kubwa ambayo imefanyika katika ujenzi wa chuo kile.

Vile vile alizungumza suala la serikali ya wanafunzi. Ni kwamba Mhe. Haji tusiwe na wasi wasi na serikali za wanafunzi, kwa kweli zinatusaidia sana na sasa hivi hata ninapofanya ziara nikenda kwenye maskuli, basi hutambulishwa kama huyu ndiye Rais, huyu ndiye Waziri Kiongozi. Wale wanafunzi wenyewe sasa wanaanza kujengwa wakiwa katika mazingira yale ya kuelewa kama kuna nafasi hizo. Kwa hivyo, tusiwe na mashaka nafasi za Ubunge na Uwakilishi zitakuja kujazwa na hao hao baadae, basi ni vizuri tukawapa ujuzi na mapema.

Lakini kuhusu suala la maandamano na mambo mengine ni kwamba hapa Zanzibar *alhamdulilah* suala hilo halipo, kuna utulivu kwa wanafunzi na hata

walimu ingawa wanasikitika kwamba si mahali pake sana kulisema hapa kwa sababu tunazungumza mambo ya mswada lakini katika hali hiyo ya maandamano na uchochezi ambao unafanywa. Naskia kuna warka umetolewa na chama cha walimu *ZATU* kuwataka walimu washiriki katika kutia saini na kulalamika kwamba wana kero nyingi sana ambazo hazijatekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu nikohowe hapa hapa ili taarifa ziwafike, najua wizara yangu inafanya jukumu la kutoa taarifa kamili. Kumetolewa warka kutaka walimu waliokuwa wanachama wa *ZATU*, na waliokuwa sio wanachama kulalamikia asilimia 25, mambo ya nauli na kuondoshwa kwa Chuo cha Ualimu cha Nkuruma. Nasikitika sana kwamba *ZATU* wote ni walimu, na kumbe hawajui kile ambacho wanakifanya. Mhe. Mwenyekiti, posho la asilimia 25 , Mheshimiwa niliwasilisha bajeti mbele ya Baraza lako tukufu na Waheshimiwa Wajumbe wote wamenisikia kwamba suala hilo serikali imeliangalia na *inshaallah* katika marekebisho ambayo tunarajia yatafanyika wakati wowote kuanzia *January* basi mambo haya yatakaa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, kilichokuwa kinatafutwa hapa walijua kwamba serikali itafanya marekebisho basi kujipa sifa wao ni kwamba wametoa shindikizo, ndio serikali ikatekeleza. Kwa hivyo, mimi nawaambia wamechelewa sana bahati mbaya.

Mhe. Mwenyekiti, jengine hili la nafasi ya mafunzo ya ualimu katika Chuo cha Nkuruma, mafunzo yapo, na hakuna mwanafunzi yoyote aliyeomba nafasi ya Diploma akakosa, labda kuwe kuna tatizo jengine. Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi huwa wanapelekwa Chuo cha Kiislamu, wanapelekwa Chuo cha Benjamin Mkapa na wengine wanapelekwa Chuo cha Kiislamu Kiuyu. Pia tumepandisha daraja kwani hivi sasa Diploma inaanza kutolewa *SUZA* mambo ya *Compyuter science* na *inshaallah* mipango iko karibu kutekelezwa kuanzisha Diploma ya sayansi hapo hapo.

Kwa hivyo, badala ya kupongeza wao wamelaumu, na mafunzo hayo yatatolewa hapo hapo Nkuruma. Kuhusu nauli za walimu ni kwamba nauli zote zinatolewa kwa wakati na sasa hivi hakuna anayetudai hata mmoja, tunalipa karibu milioni 39 kila mwezi, nauli za walimu. Kwa hivyo, *ZATU* kabla ya kuchukua hatua kama hiyo wangekuja tukawapa maelekezo, kama walivyofanya wenzao, Maimamu na Mashekhe wale wa Uamsho na wengineo, nawapongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, wao waliposikia kuna jambo fulani kuhusu Chuo cha Kiislamu walikuja, na nimezungumza nao vizuri na mwisho wakaniombea dua kubwa sana, nawashukuru. Tatizo lao wao ni kwamba walisikia tu Chuo cha Kiislamu sasa kimebadilishwa kitaitwa Mazizini Secondary School, walitaka

jina la Chuo cha Kiislamu libakie, mimi nikawaambia hatukufuta jina, na mafunzo yapo basi tukaondoka tumefahamiana vizuri. Kwa hivyo, ni vizuri na *ZATU* kama wangekuwa na tatizo kama hilo basi wangekuja tukaelewana.

Mhe. Mwenyekiti, napenda niwaambie walimu wangu kwamba, wasije wakasaini waraka ule kwa sababu ule ni warka ambao una nia ya kupotosha jamii kuona kwamba serikali haiko makini kwa jambo hilo. Mimi nawaomba sana walimu wangu wasisaini waraka huo, wale wanachama na wasiokuwa wanachama kwa sababu lengo la warka ilikuwa ni kupotosha zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na hoja iliyokuwepo mbele yetu ni kwamba namwambia Mhe. Haji tusiwe na wasi wasi, vijana hawa wa Zanzibar ni makini na nawaasa wawe makini zaidi wasije wakaingia katika matatizo yaliyokuwa hayapo.

Pia Mhe. Haji ameelezea kwamba hakuna kitivo chochote cha Chuo Kikuu hapa Zanzibar cha Jamhuri ya Muungano, ni kwamba kitivo kipo. Kile Chuo cha Taasisi ya Bahari kilichokuwepo pale Forodhani, kile ni chuo cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kiko chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaama na tayari kuna eneo la Buyu mipango iko tayari, ni kweli tukubali kwamba miaka imekuwa mingi, nafikiri karibu miaka 15 hata ile alama ya ujenzi sasa hivi imeanza kupotea. Lakini hivi karibu mimi niliwahi kuzungumza na Waziri anayehusika na aliniahidi kwamba itatengwa bajeti maalum kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Chuo hicho cha Sayansi ya Baharini.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Haji kwamba hakuna kero, vijana wetu wa Zanzibar wote wanapata nafasi hapa Zanzibar, Tanzania Bara, na nje ya Tanzania na wengi wao wanakwenda Uganda kwa sababu kule kidogo masharti ni nafuu ya kujiunga. Na hata nje hivi sasa tuna wanafunzi zaidi ya 237 waliokuwa nje ya nchi ya Tanzania wanasoma mafunzo mbali mbali ya shahada ya kwanza, pili na tatu.

Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim alichangia mswada huu, mimi napenda nimuhakikishie kwamba tukijaaliwa wiki ya mwisho ya Novemba tutakuwa na sherehe za Elimu bila ya Malipo, tumechelewa kwa sababu ya mwezi mtukufu wa ramadhani na mambo yalikuwa mengi. Kwa hivyo, maktaba tukijaaliwa itafunguliwa rasmi katika sherehe hizo, pamoja na siku ya walimu duniani, na siku hiyo ndio tutawapa maelezo mazuri walimu wetu. Kwa hivyo, napongeza juhudi kubwa iliyopatikana hapo.

Mhe. Mustafa amesema kwamba hakuna sifa za Naibu Makamo Mkuu wa Chuo. Mhe. Mustafa tizama sheria hiyo kifungu cha 10 (3) kinaeleza awe na uzoefu wa miaka 7 na mambo mengineyo yanayohusiana na sifa kama hizo.

Mhe. Mzee Ali Ussi, yeye amepongeza na amekubaliana na hayo lakini kidogo yeye aliangalia sheria ya zamani kwa sababu sheria ya sasa ndio imerekebisha hayo, kwamba tuwe na wataalamu wenye mambo ya *Professor*, hayo ndio yamerekebishwa kwa mujibu wa sheria hii mpya. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale ambao wanakubaliana na hoja hii wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa na kuafikiwa)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima, ili kupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Nam. 8 ya 1999

Kifungu cha 1	Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 2	Kusomwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 3	Marekebisho ya kifungu cha pili
Kifungu cha 4	Marekebisho ya kifungu cha kumi pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Moh'd Ali Salim: Mhe. Mwenyekiti, ni jambo dogo sana lakini nadhani Mhe. Waziri hakufahamu, vile nilivyokusudia kuzungumza. Katika kifungu hiki cha 4 katika uteuzi wa Naibu Makamo Mkuu wa Chuo, hawa ni wawili, kuna wa utawala na yule wa taaluma. Nililokusudia ni kuwa huyu anateuliwa kuwa wa utawala mwengine anateuliwa ni wa taaluma, amekaa kipindi chake cha kwanza amemaliza, na ameteuliwa tena kipindi cha pili. Je, huyu ataweza tena kuteuliwa kwenye utawala kwa sababu pale mwanzo hakuteuliwa kwenye utawala, aliteuliwa kwenye taaluma. Hilo ndilo nililokusudia.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tunazungumza lugha moja, mama unaweza kumwita Bimkubwa wakati ndio huyo huyo. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba hakuna tatizo kitu kinachohitajika tukihisi kwamba anaweza kutusaidia zaidi upande mwengine basi hilo litawezekana hakuna matatizo. Lamsingi tunachotaka kuwa na viongozi ambao wamekomaa katika maeneo yao kama kwenye utawala amefanya vizuri basi ataendelea kuwa kwenye utawala au kwenye taaluma.

Mhe. Moh'd Ali Salim: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee

Kifungu 4	Marekebisho ya kifungu cha kumi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 5	Kufutwa kwa kifungu cha 11
Kifungu 6	Marekebisho ya kifungu cha 12 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 7	Marekebisho ya kifungu cha 16
Kifungu 8	Marekebisho ya kifungu cha 18 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 9	Marekebisho ya kifungu cha 26 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 10	Marekebisho ya kifungu cha 37 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 11	Marekebisho ya kifungu cha 40 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 12	Marekebisho ya kifungu cha 41 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 13	Marekebisho ya jadweli la kwanza pamoja na marekebisho yake
Kifungu 14	Marekebisho ya jadweli la kwanza pamoja na marekebisho yake
Kifungu 15	Marekebisho ya jadweli la pili pamoja na marekebisho yake
Kifungu 16	Marekebisho ya jadweli la pili pamoja na marekebisho yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu baada ya kifungu, na kukubali pamoja na masahihisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Nam.8 ya 1999

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii wanyanyue mikono, wasiokubali. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

KUAKHIRISHWA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi kwa kuwa tumemaliza shughuli zetu mapema naomba uliahirishe Baraza lako tukufu hadi kesho siku ya Alhamis saa 3:00 asubuhi.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii wanyanyue mikono, wasiokubali. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 5:00 asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 29-10-2009 saa 3:00 asubuhi)